SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS FEDHA NA MIPANGO

JAMAL KASSIM ALI (MBM)

AKIWASILISHA MAPENDEKEZO YA SERIKALI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022.

YALIYOMO

I. UTANGULIZI 1
II. TATHMINI YA MWENENDO WA HALI YA UCHUMI 3
III. TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA KIPINDI CHA MIEZI TISA (JULAI 2020 – MACHI 2021) 8
A. MAKADIRIO YA MAPATO 9
B. UTEKELEZAJI HALISI WA MAPATO YA SERIKALI JULAI 2020 HADI MACHI 2021 10
C. UKUSANYAJI WA MAPATO KITAASISI 10
I. Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) 10
II. Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) - Zanzibar 10
III. Kodi ya Mapato kwa Wafanyakazi wa SMT 11
MAPATO YA MFUKO WA MIUNDOMBINU 12
IV. UTEKELEZAJI WA HATUA ZA KUIMARISHA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 12
A. HATUA ZINAZOHUSU MAREKEBISHO YA SHERIA 12
B. HATUA ZA KUIMARISHA USIMAMIZI, UKUSANYAJI NA UTAWALA WA KODI 16
A. MAKADIRIO YA MATUMIZI 18
B. UTEKELEZAJI HALISI WA MATUMIZI YA SERIKALI KWA KIPINDI CHA JULAI 2020 HADI MACHI 2021 18
I. MATUMIZI YA HUDUMA ZA MFUKO MKUU 19
II. MATUMIZI YA MFUKO WA MIUNDOMBINU 20
III. DENI LA TAIFA 20
V. MATARAJIO YA MAPATO NA MATUMIZI JULAI 2020 HADI JUNI 2021 21
A. MATARAJIO YA MAPATO JULAI 2020-JUNI 2021 21
B. MATARAJIO YA MATUMIZI JULAI 2020-JUNI 2021 23
VI. SERA ZA BAJETI NA MIKAKATI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 24
VII. MAPENDEKEZO YA HATUA ZA KUIMARISHA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 25
A. HATUA ZINAZOHUSU MAREKEBISHO YA SHERIA 26

B. HATUA ZA KUIMARISHA USIMAMIZI NA UTAWALA WA KODI..... 34
VIII.SURA YA BAJETI..... 36
A. MAKADIRIO YA MAPATO 36
B. MAKADIRIO YA MATUMIZI..... 38
IX. MWELEKEO WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2021/22 -2023/24..... 43
A. SHABAHA NA MALENGO YA UCHUMI KWA MWAKA 2021-2023..... 43
X. VIPAUMBELE VYA KITAIFA KWA MWAKA 2021/2022..... 45
XI. SHUKURANI..... 46
XII. HITIMISHO 49

I. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** Kwanza kabisa, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu Mwenye Ukarimu aliyetujaalia uzima wa afya na amani katika nchi yetu, kwa kutuwezesha kuwa pamoja leo hii Wajumbe wa vyama vitatu tukiwa wenye furaha na utulivu mbele ya Baraza hili tukufu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu atuzidishie umoja, mshikamano, hekima na busara katika kutimiza wajibu wetu wa kujadili, kushauri na hatimae kuidhinisha Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali ili yawe muongozo wa utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

2. **Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Katiba yetu ya Zanzibar ya mwaka 1984 na Sheria ya Fedha za Umma namba 12 ya mwaka 2016 zinampa wajibu wa kisheria Waziri mwenye dhamana ya Fedha kutayarisha na kuwasilisha mbele ya Baraza la Wawakilishi Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali. Fursa hii ndio inayoniwezesha leo hii kuwepo hapa mbele ya Baraza lako tukufu kutimiza wajibu huo ulio chini ya Kifungu 105 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 (kama ilivyorekebishwa) na Kifungu cha 41(3) cha Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2016.

3. **Mheshimiwa Spika,** Nina wajibu mkubwa wa kutoa shukrani zangu za dhati na za kipekee kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi, kwa bidii na jitihada zake katika kuiletea nchi yetu utulivu wa kisiasa na kijamii kupitia maridhiano baina ya vyama vya siasa yaliyopelekea kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa (GNU). Tuendelee kumuomba Mwenyezi Mungu, ampe uwezo, busara na hekima katika kuyadumisha mafanikio hayo kwa manufaa ya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla.

4. **Mheshimiwa Spika,** Kwa dhati kabisa napenda kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu

Hassan kwa kushika wadhifa huo kufuatia kifo cha Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli (Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi – Amen). Kwa mara ya kwanza, Taifa letu limepata kiongozi mwanamama ambae ameanza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa. Aidha, nachukua fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Dkt Philip Isdori Mpango kwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Othman Masoud Othman, Makamo wa Kwanza wa Rais na Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdullah, Makamo wa Pili wa Rais kwa kuaminiwa na kuteuliwa kuwa wasaidizi wakuu wa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

5. **Mheshimiwa Spika,** Naomba na mimi nitumie fursa hii, kuungana na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama Samia Suluhu Hassan pamoja na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi kutoa mkono wa pole kwa ndugu, jamaa na wananchi wote kufuatia vifo vya viongozi wetu wa ngazi za juu, wazalendo, wachapakazi, waadilifu na wana mapinduzi. Hayati Dkt.John Joseph Pombe Magufuli na Hayati Maalim Seif Sharif Hamad aliyekua Makamo wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar. Kwa pamoja tuwaombee Mwenyezi Mungu awape malazi pema peponi – Amen. Mbali na misiba hiyo mizito Watanzania tumeendelea kuionesha dunia kiwango chetu cha juu cha utulivu, upendo na udugu na tunaendelea kuyaishi maisha yao kwa vitendo na kutimiza ndoto zao kwa yale waliyotamani kuwafanyia wananchi.

6. **Mheshimiwa Spika,** Hotuba hii inawasilisha Bajeti ya Kwanza ya Serikali ya awamu ya Nane inayoongozwa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Hassana Mwinyi, kupitia kaulimbiu yake ***"Yajayo ni Neema Tupu".*** Serikali inawasilisha Bajeti hii ikiwa na dhamira ya dhati ya kutekeleza ahadi zilizoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 - 2025, ambayo ni tafsiri ya Dira ya Maendeleo

2020 - 2050 na Mpango wa Maendeleo wa Muda wa Kati 2021 - 2025.

II. TATHMINI YA MWENENDO WA HALI YA UCHUMI

7. **Mheshimiwa Spika,** Tokea Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa na utaratibu wa kuandaa mipango endelevu katika vipindi husika yenye lengo la kuendelea kukuza uchumi, kupunguza umasikini na kuinua ustawi wa jamii kwa wananchi wake. Katika kufanikisha azma hiyo Serikali ilizindua Dira yake ya Maendeleo 2000 - 2020 iliyokua na lengo la kuondoa umaskini uliokithiri na kuipeleka Zanzibar kufikia kiwango cha nchi zenye Uchumi wa Kipato cha Kati (Middle Income Status).

8. **Mheshimiwa Spika,** Dira 2020 ilitafsiriwa katika Mpango wa Kupunguza Umasikini Zanzibar (ZPRP) na Mikakati ya Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar Awamu ya Kwanza hadi ya Tatu (MKUZA I, MKUZA II na MKUZA III) ambayo ilitumika kama nyenzo za utekelezaji wake na kuiwezesha Zanzibar kupata mafanikio niliyoyaainisha.

9. **Mheshimiwa Spika,** Kama tunavyofahamu, katika kipindi cha mwaka 2020, dunia ilikumbwa na janga kubwa la maradhi ya korona yaliyopewa jina la COVID 19 ambayo yalioanzia katika mji wa Wuhan nchini China na kusambaa kwa kasi kubwa katika maeneo yote duniani. Kuwepo kwa janga la korona kumechangia kwa kiasi kikubwa kuporomoka kwa uchumi wa dunia kutokana na sababu mbali mbali zinazoshabihiana ikiwemo kuzorota kwa uwekezaji na utalii, kufungwa kwa biashara na uzalishaji viwandani, kushuka kwa bei za nishati, kuongezeka kwa matumizi makubwa ya Serikali katika kuhakikasha inasimamia huduma za afya na kupunguza matumizi katika miradi ya maendeleo, kupotea kwa ajira na kuwepo kwa vifo vya watu wengi duniani.

10. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha mwaka 2020, uchumi wa dunia ulifikia wastani wa asilimia -3.3 kutoka ukuwaji wa wastani wa asilimia 2.8 mwaka 2019, Uchumi wa nchi zilizoendelea umefikia wastani wa asilimia -4.7 mwaka 2020 kutoka ukuwaji wa wastani wa asilimia 1.6 mwaka 2019, na kwa nchi zenye uchumi unao ibukia, uchumi wanchi hizo umefikia wastani wa asilimia -2.2 mwaka 2020 kutoka ukuaji wa wastani wa asilimia 3.6 mwaka 2019.

11. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Afrika, kasi ya ukuaji uchumi imeporomoka kufikia wastani wa asilimia 2.1 mwaka 2020 kutoka ukuwaji wa wastani wa asilimia 3.3 mwaka 2019. Katika bara la Afrika, ni nchi kumi na moja (11) tu ndizo zilioenyesha ukuaji katika kipindi cha mwaka 2020 zikiwemo Zanzibar, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Djibuti, Ethiopia, Kenya, Tanzania, Egypt, Malawi, Benini, Guinea, Niger na Togo.

Mafanikio ya Kiuchumi kwa Zanzibar

12. **Mheshimiwa Spika,** Pato halisi la Taifa limeendelea kuwa zuri ambapo kwa mwaka 2020 lilifikia thamani ya TZS 3,116 bilioni ikilinganishwa na thamani ya TZS 3,078 bilioni mwaka 2019. Aidha, Pato la Taifa kwa bei za soko limefikia thamani ya TZS 4,209 bilioni mwaka 2020 kutoka thamani ya TZS 4,136 bilioni mwaka 2019.

13. **Mheshimiwa Spika,** Kasi ya ukuaji huu imepelekea Pato la Mwananchi kufikia wastani wa Shilingi 2.53 milioni sawa na Dola za kimarekani 1,099 kutoka Shilingi 2.55 milioni sawa na Dola 1,115. Kipato hiki kimeifanya Zanzibar iendelee kubaki katika nchi za uchumi wa kiwango cha chini cha kati.

Matokeo yaliyotokana na ukuaji wa Uchumi kwa mwaka 2020

14. **Mheshimiwa Spika,** Miongoni mwa matokeo yaliyopatikana kwa kuendelea kukua kwa uchumi ni kama yafuatayo;

Mfumko wa Bei

15. **Mheshimiwa Spika,** Kuendelea kuwepo kwa utulivu wa bei za bidhaa na huduma ambapo katika kipindi cha mwaka 2020 kasi ya mfumko wa bei ulikuwa chini ya wastani wa asilimia 5, kama ni kigezo kimoja wapo cha upimaji wa ukuaji uchumi katika nchi wanachama wa Jumuia ya Afrika Mashariki.

Ajira

16. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha mwaka 2020, jumla ya ajira zilizopatikana katika sekta za umma na binafsi zilifikia 67,095 kutoka ajira 62,804 mwaka 2019.

Huduma za Afya

17. **Mheshimiwa Spika,** Wataalamu katika sekta ya afya wameongezeka, ikijumuisha madaktari bingwa kutoka 57 mwaka 2019 hadi 64 mwaka 2020, madaktari wa kawaida kutoka 247 mwaka 2019 hadi 270 mwaka 2020. Aidha, watoa huduma na wauguzi wamepungua kutoka 1,385 mwaka 2019 hadi 1,342 mwaka 2020.

18. **Mheshimiwa Spika,** Idadi ya wagonjwa waliolazwa hospitali na vituo vya afya kutibiwa na kurudi nyumbani imepungua kutoka jumla ya wagonjwa 1,934,419 mwaka 2019 hadi kufikia 1,849,716 mwaka 2020 sawa na upungufu wa asilimia 4.4. Wagonjwa waliolazwa hospitali na vituo vya afya imepungua kutoka 96,055 mwaka 2019 hadi 95,844 mwaka 2020 sawa na upungufu wa asilimia 0.22.

19. **Mheshimiwa Spika,** Idadi ya vituo vya afya vya Serikali imeongezeka kutoka 167 mwaka 2019 na kufikia 170 mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 1.8. Aidha, kwa upande wa vituo vya afya vya binafsi vimeongezeka kutoka 96 mwaka 2019 hadi 117 mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 21.9.

Huduma za Elimu

20. Mheshimiwa Spika, Utoaji wa huduma za Elimu kwa mwaka 2020 umeimarika kama ifuatavyo:

Idadi ya skuli za Serikali katika kiwango cha elimu ya maandalizi, msingi na sekondari imeongezeka mwaka 2020.
Skuli za maandalizi za Serikali imeongezeka kutoka 30 mwaka 2019 hadi 35 mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 16.7;
Skuli za msingi zimeongezeka kutoka skuli 266 mwaka 2019 hadi skuli 293 mwaka 2020 sawa na ongezeko la asilimia 10.2; na
Kwa upande wa skuli za sekondari zimeongezeka kutoka skuli 169 mwaka 2019 na kufikia skuli 210 mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 24.3.

21. Mheshimiwa Spika, Idadi ya wanafunzi wanaosoma Elimu ya Msingi katika Skuli za Serikali na binafsi imeongezeka na kufikia 316,097 mwaka 2020 kutoka 290,510 mwaka 2019 sawa na ongezeko la asilimia 8.8. Idadi ya wanafunzi wa Elimu ya Msingi katika skuli za Serikali imefikia 278,580 mwaka 2020 kutoka wanafunzi 257,453 mwaka 2019 sawa na ongezeko la asilimia 8.2 Aidha, idadi ya wanafunzi wa Elimu ya Msingi katika skuli binafsi imefikia 37,517 mwaka 2020 kutoka 33,057 mwaka 2019 sawa na ongezeko la asilimia 13.5.

Ukuaji wa Sekta katika Pato la Taifa

22. Mheshimiwa Spika, Mafanikio mengine ya kiuchumi yanabainika katika Sekta za uzalishaji yakiwemo yafuatayo:

Sekta ya Huduma

23. Mheshimiwa Spika, Sekta ya Huduma inajumuisha sekta ndogo za Malazi na Huduma za Chakula, Sanaa, Burdani na Ubunifu, Afya, Elimu, Mawasiliano n.k. Ukuaji wa Sekta ya Huduma katika Pato

la Taifa kwa mwaka 2020 ulifikia wastani wa chini ya asilimia 1.0 ikilinganishwa na ukuaji wa wastani wa asilimia 8.7 mwaka 2019. Kupungua kwa ukuaji wa Sekta hii kumesababishwa zaidi kwa kupungua kwa sekta ndogo ya Malazi na huduma za chakula kutoka asilimia 20.2 mwaka 2019 na kufikia asilimia 15.8 mwaka 2020, ambapo jumla ya watalii waliongia nchini wamepunguwa kwa asilimia 51.6 na kufikia watalii 260,644 kutoka watalii 538,264 waliongia nchini mwaka 2019.

24. **Mheshimiwa Spika,** Nchi zilizoingiza watalii wengi katika kipindi hiki ni Urusi asilimia 16, Ufaransa asilimia 8.5, Italia asilimia 8.2 na Bara la Amerika asilimia 6.2.

Sekta ya Viwanda

25. **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Viwanda inajumuisha sekta ndogo ya uzalishaji viwandani, ujenzi, uchimbaji mawe na mchanga n.k. Kwa mwaka 2020, Sekta hii imekua kwa kasi ya asilimia 5.2 ikilinganishwa na asilimia 10.6 mwaka 2019. Kupungua kwa ukuaji katika Sekta hii kumesababishwa na kuanguka kwa Sekta ndogo ya uzalishaji viwandani kutoka wastani wa asilimia 20.5 mwaka 2019 na kufikia wastani wa asilimia 6.5 mwaka 2020. Vile vile, Sekta ndogo ya usambazaji maji safi na uchukuzi wa maji taka ukuaji wake umeshuka na kufikia wastani wa asilimia 2 mwaka 2020 kutoka wastani wa asilimia 12.6 mwaka 2019.

Sekta ya Kilimo

26. **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Kilimo inajumuisha sekta ndogo za mazao, uvuvi, mifugo na misitu. Katika mwaka 2020 ukuaji wa sekta hii katika Pato la Taifa umefikia wastani wa asilimia 3.3 kutoka ukuaji wa wastani wa asilimia 2.6 mwaka 2019. Ukuaji katika sekta ya kilimo umetokana na kuongezeka kwa uzalishaji katika sekta ndogo ya mazao kutoka wastani wa asilimia -5.8 mwaka 2019 na kufikia wastani wa asilimia 1.3 mwaka 2020. Aidha, sekta ndogo ya

uvuvi uzalishaji wake umeongezeka na kufikia wastani wa asilimia 3.5 mwaka 2020 kutoka wastani wa asilimia 3.3 mwaka 2019.

III. TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA KIPINDI CHA MIEZI TISA (JULAI 2020 – MACHI 2021)

A. Makadirio ya Mapato

27. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2020/2021 Serikali imekadiria kukusanya jumla ya TZS 1,579.2 bilioni, ambapo Baraza lako tukufu liliidhinisha makadirio hayo katika maeneo yafuatayo:

a. Mapato ya ndani ya jumla ya TZS 1,050 bilioni;
b. Mikopo ya ndani ya TZS 45 bilioni;
c. Ruzuku ya Mfuko wa Pamoja na Washirika wa Maendeleo (basket fund) TZS 3.8 bilioni;
d. Ruzuku na Mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo jumla ya TZS 412.6 bilioni ikiwemo mikopo ya TZS 340.5 bilioni na TZS 72.1 bilioni ruzuku; na
e. Marejesho ya TZS 61 bilioni ikiwa ni sehemu ya Ujenzi wa Terminal III kutoka Benki ya Exim ya China.

28. **Mheshimiwa Spika,** Kati ya mapato ya ndani ya TZS1,050.0 bilioni, jumla ya TZS 921.3 bilioni zilitarajiwa kupatikana kutokana na makusanyo ya vyanzo vya kodi na TZS 128.7 bilioni ni kutokana na vyanzo visivyo vya kodi kwa mgawanyo ufuatao:

a. Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) TZS 516.7 bilioni sawa na asilimia 49.2 ya makadirio ya mapato ya ndani;
b. Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) TZS 383.5 bilioni sawa na asilimia 36.5 ya makadirio ya mapato ya ndani;
c. Mapato ya Wizara TZS 104.7 bilioni sawa na asilimia 9.9 ya makadirio ya mapato ya ndani;
d. Kodi ya Mapato kwa wafanyakazi wa SMT TZS 21.0 bilioni sawa na asilimia 2 ya makadirio ya mapato ya ndani;
e. Gawio la faida kutoka Benki Kuu (BoT) TZS 13.5 bilioni sawa na asilimia 1.3 ya makadirio ya mapato ya ndani; na

f. Gawio la faida kutoka katika Mashirika ya SMZ TZS 10.5 bilioni sawa na asilimia 1 ya makadirio ya mapato ya ndani.

B. Utekelezaji Halisi wa Mapato ya Serikali Julai 2020 hadi Machi 2021

29. Mheshimiwa Spika, Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai- Machi) Jumla ya Mapato yamefikia TZS 723.3 bilioni sawa na asilimia 61 ya makadirio ya TZS 1,185.1 bilioni kwa kipindi hicho na asilimia 45.8 kwa kipindi cha mwaka kwa mchanganuo ufuatao:

a. Mapato ya Ndani

30. Mheshimiwa Spika, Mapato ya ndani hadi Machi 2021 yamefikia TZS 524.1 bilioni, sawa na asilimia 64 ya makadirio ya TZS 819.2 bilioni kwa kipindi hicho na asilimia 33.2 kwa makadirio ya mwaka.

31. Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha mapitio mapato ya ndani ya TZS 524.1 bilioni yanamaanisha upungufu wa asilimia 19.1 ikilinganishwa na makusanyo ya TZS 648.2 bilioni zilizokusanywa kipindi kama hicho mwaka 2019/2020. Kati ya makusanyo hayo, mapato ya kodi yalifikia TZS 453.5 bilioni ambazo ni sawa na asilimia 63.0 ya makadirio ya TZS 720.4 bilioni. Mapato hayo yanaonesha upungufu wa asilimia 18.4 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2019/2020 ambapo jumla ya TZS 555.5 bilioni zilikusanywa.

32. Mheshimiwa Spika, Mapato yasiyokuwa ya kodi yalifikia TZS 70.7 bilioni sawa na asilimia 71.6 ya makadirio ya TZS 98.7 ya kipindi hicho. Kiasi hicho kinamaanisha upungufu wa asilimia 23.7 ikilinganishwa na makusanyo ya TZS 92.8 bilioni yaliyopatikana kipindi kama hicho mwaka 2019/2020.

C. Ukusanyaji wa Mapato Kitaasisi

I. Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB)

33. Mheshimiwa Spika, Ukusanyaji wa Mapato ya ndani Kitaasisi, Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021, Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) ilikusanya jumla ya TZS 223.3 bilioni sawa na asilimia 53.9 ya makadirio ya TZS 414.1 bilioni katika kipindi hicho na asilimia 43.2 kwa makadirio ya mwaka. Mapato hayo yanaonesha upungufu wa asilimia 29.5 ikilinganishwa na makusanyo ya TZS 316.8 bilioni kwa kipindi kama hicho kwa mwaka 2019/2020.

II. Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) - Zanzibar

34. Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mapato Tanzania - Zanzibar (TRA) ilikusanya jumla ya TZS 209.1 bilioni sawa na asilimia 73.3 ya makadirio ya TZS 285.3 bilioni katika kipindi hicho na asilimia 55 ya makadirio ya mwaka. Mapato hayo yanaonesha upungufu wa asilimia 6.2 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2019/20 ambapo jumla ya TZS 222.9 bilioni zilikusanywa.

III. Kodi ya Mapato kwa Wafanyakazi wa SMT

35. Mheshimiwa Spika, Makusanyo ya Kodi ya Mapato kutoka kwa wafanyakazi wa SMT waliopo Zanzibar yalifikia TZS 21 bilioni sawa na bajeti yote iliyopangwa kwa mwaka.

b. Mkopo wa Ndani

36. Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa mikopo ya ndani kwa kipindi cha miezi tisa ilifikia jumla ya TZS 52.1 bilioni sawa na asilimia 115.8 ya makadirio ya TZS 45.0 bilioni ya mwaka.

c. Mapato kutoka kwa Washirika wa Maendeleo

37. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai-Machi 2020/2021, Serikali imepokea Jumla ya TZS 119.7 bilioni sawa na asilimia 39 ya makisio ya miezi tisa ya TZS 306 bilioni na asilimia 28.3 ya makadirio ya mwaka, kutoka kwa Washirika wa Maendeleo Kati ya fedha hizo Ruzuku TZS 13.3 bilioni, kiasi hicho cha ruzuku (TZS 2.6 bilioni kutoka mfuko wa Pamoja na washirika wa Maendeleo (basket fund)) na Mikopo ya TZS 106.4 bilioni kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi na Programu za Maendeleo.

Mapato ya Mfuko wa Miundombinu

38. **Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka 2020/2021 Jumla ya TZS 44.5 bilioni zilikadiriwa kukusanywa kutoka Mfuko wa Miundombinu ambapo TZS 16.8 bilioni kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na TZS 27.7 bilioni kutoka Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB).

39. **Mheshimiwa Spika,** Jumla ya mapato yaliyopokelewa kutokana na Mfuko wa Miundombinu kwa kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021 yamefikia TZS 23.1 bilioni sawa na asilimia 64 ya makadirio ya TZS 34.7 bilioni. Kati ya fedha hizo, TZS 15.2 bilioni zimekusanywa na ZRB sawa na asilimia 69 ya makadirio ya TZS 22.1 na TRA imekusanya TZS 7.9 bilioni sawa na asilimia 62 ya makadirio ya TZS 12.6 bilioni.

d. Mapato mengineyo

40. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa mapato mengineyo jumla ya TZS 28.3 bilioni zimepatikana ikihusisha msaada wa kibajeti (GBS) TZS 9.5 bilioni, mkopo wa dharura TZS 6.9 bilioni na TZS 10.9 bilioni zinatokana na “Bank facilities services”.

IV. UTEKELEZAJI WA HATUA ZA KUIMARISHA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

41. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2020/21, Baraza la Wawakilishi liliridhia mapendekezo ya Serikali ya kuchukua hatua kadhaa ili kuimarisha usimamizi na ukusanyaji wa Mapato ya Serikali. Hatua hizo zilihusisha marekebisho ya Sheria pamoja na Kuimarisha Usimamizi na Utawala wa Kodi.

Muhtasari wa utekelezaji wa hatua hizo ni kama ifuatavyo;

A. Hatua Zinazohusu Marekebisho ya Sheria

i. Kufanya Marekebisho katika Sheria ya Ongezeko la Thamani (VAT);

a) Kupunguza Kiwango cha VAT

42. Mheshimiwa Spika, Baraza lako tukufu liliridhia kupunguza kiwango cha VAT kutoka 18% hadi 15% ili kukabiliana na janga la maradhi ya korona. Utekelezaji wa hatua hii ulianza rasmi mwezi Julai 2020.

b) Kutoa Msamaha wa VAT kwenye Vifaa vya Uvuvi

43. Mheshimiwa Spika, Sheria husika imefanyiwa marekebisho kwa kutoa unafuu wa kodi ya VAT wakati wa uingizaji wa boti kubwa za kuanzia urefu wa mita 18 na zaidi, mashine za boti, pamoja na vifaa vyengine vya uvuvi vinavyoingia nchini ili kuimarisha sekta ndogo ya uvuvi pamoja kuongeza kipato cha mwananchi kwa kujikwamua na umasikini. Utekelezaji wa hatua hii ulianza rasmi mwezi Julai 2020.

c) Kupandisha Kiwango cha Mauzo Ghafi kwa Usajili wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT)

44. **Mheshimiwa Spika,** Baraza la Wawakilishi liliridhia marekebisho ya kanuni ya sheria ya VAT kwa kuongeza kiwango cha usajili wa VAT kutoka mauzo ghafi milioni 30 hadi 50 ili kuendana na mabadiliko makubwa ya kiuchumi yanayoendelea pamoja na kwenda sambamba na mabadiliko yaliyopendekezwa ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) ya kuwa na kiwango cha chini cha USD 25,000.

45. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2021, jumla ya Wafanyabishara 132 wamesajiliwa katika wigo wa VAT na TZS 590 Milioni zimekusanywa kutokana na marekebisho ya sheria hiyo.

ii. Marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Hoteli Na. 1 ya Mwaka 1995;

46. **Mheshimiwa Spika,** Sheria husika imefanyiwa marekebisho kwa kupunguza kiwango cha kutozea kodi kutoka 18% hadi 12% ili kukabiliana na athari za janga la maradhi ya korona katika uchumi. Hatua hii imezingatia kuwa walipa kodi wa Ushuru wa hoteli hawana fursa ya kujirejeshea VAT wanayolipa kwenye ununuzi wao hivyo ni gharama kwao. Utekelezaji wa hatua hii ulianza rasmi mwezi Julai 2020.

iii. Kufanya Marekebisho katika Sheria ya Ada ya Huduma za Bandari Nam. 2 ya mwaka 1999;

47. **Mheshimiwa Spika,** Baraza lako tukufu liliridhia marekebisho ya Sheria husika kwa kuondoa Ada ya kodi ya miundombinu na Tozo ya Mamlaka ya Usafiri Baharini (marinetime levy) wakati wa ukokotoaji wa Ada ya usafirishaji baharini ili kuondoa malalamiko pamoja na kuhakikisha kuwa mfumo wa kodi unakuwa sawa na haki kwa walipa kodi wote. Utekelezaji wa hatua hii ulianza rasmi mwezi Julai 2020.

iv. Kufanya Marekebisho katika Sheria ya Usimamizi wa Kodi (TAPA) Nam. 7 ya mwaka 2009.

a) Kuongeza Kipengele cha Pingamizi za Kodi (Tax Objection) katika Sheria ya Usimamizi wa Kodi (TAPA) Nam. 7 ya mwaka 2009.

48. Mheshimiwa Spika, Sheria husika imefanyiwa marekebisho kwa kuongeza kipengele cha pingamizi za kodi (Tax objection) kwa walipakodi dhidi ya Kamishna ili kumpa haki mlipakodi kupinga maamuzi yaliyotelewa na Kamishna mbali na maamuzi ya awali ya makadirio ya mapato.

b) Kumpa Uwezo Waziri Kuongeza Muda wa Kuwasilisha Ritani na Malipo ya Kodi Wakati wa Matukio Yasiyotarajiwa.

49. Mheshimiwa Spika, Baraza la Wawakilishi liliridhia marekebisho ya Sheria husika kwa kumpa uwezo Waziri anaeshughulikia masuala ya fedha kuongeza muda wa kuwasilisha ritani na malipo ya kodi kwa mlipakodi wakati wa matukio yasiyotarajiwa. Utekelezaji wa hatua hizo ulianza rasmi mwezi Julai 2020, na hakukuwa na athari yoyote iliyojitokeza katika ukusanyaji wa mapato.

v. Kufanya Marekebisho katika Sheria ya Ajira Nam. 11 ya Mwaka 2005;

50. Mheshimiwa Spika, Baraza la Wawakilishi liliridhia marekebisho ya sheria husika kwa kumpa uwezo Waziri anaehusika na masuala ya Kazi kusamehe malipo ya ada ya vibali vya kazi kwa Mwajiriwa wa Kigeni katika Taasisi za Umma na Mwekezaji aliewekeza zaidi ya 20% katika Uwekezaji Mkakati (Strategic Investment) baada ya kushauriana na kukubaliana na Waziri anaeshughulikia masuala ya fedha. Utekelezaji wa hatua hii ulianza rasmi mwezi Julai 2020.

vi. Kufanya Marekebisho katika Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Nam. 12 ya mwaka 2016.

a) Udhibiti wa Utozaji wa Ada na Tozo;

51. Mheshimiwa Spika, Sheria husika imefanyiwa marekebisho kwa kuongeza kifungu cha 133B kinachompa uwezo Waziri anaeshughulikia masuala ya fedha kupitia na kuidhinisha mapendekezo ya kuanzisha, kuongeza au kufuta ada na tozo, pamoja na kutoa miongozo juu ya usimamizi wake kwa Taasisi za umma kabla ya kuanza kutumiwa na Taasisi husika ili kuimarisha usimamizi wa Ada na Tozo.

b) Utowaji wa Risiti kwa Uwasilishaji wa Fedha za Mapato ya Serikali;

52. Mheshimiwa Spika, Baraza la Wawakilishi liliridhia marekebisho ya Sheria husika kwa kuongeza kifungu kidogo kinachoweka utaratibu wa utoaji wa risiti kutokana na mapato yanayowasilishwa hazina na Taasisi za umma.

c) Kubadilisha Utaratibu wa Uzuiyaji wa Mapato kwa Taasisi za Serikali;

53. Mheshimiwa Spika, Baraza lako tukufu lilifanya marekebisho ya Sheria husika kwa kufuta mfumo wa "Appropriation - in - Aid" kwa Taasisi za umma zinazopokea ruzuku, na kutanguliza mapato yake katika Mfuko Mkuu Hazina na baadae kwenda kwa Taasisi husika ili kusimamia ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Hadi kufikia Machi 2021, Bodi ya uhaulishaji, Bodi ya Wakandarasi na Bodi ya Wasanifu zimeanza kufuata utaratibu huo.

B. Hatua za Kuimarisha Usimamizi, Ukusanyaji na Utawala wa Kodi

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)

i. Kupata taarifa kutoka kwa mtu wa tatu;

54. Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) imeendelea kushirikiana na taasisi za umma. Aidha, TRA imefanya mawasiliano na Taasisi ya Bodi ya Chakula na Madawa, Bodi ya Leseni, Bodi ya Usajili wa Vyombo vya Baharini na Msajili wa skuli binafsi kwa ajili ya kupata orodha ya watu waliowasajili na wamiliki wao pamoja na kupata taarifa sahihi za walipa kodi. Hadi kufikia Machi 2021, jumla ya TZS 354 Milioni zimekusanywa katokana na hatua hiyo.

ii. Kuharakisha Maamuzi ya Pingamizi za Kodi (Tax Objections);

55. Mheshimiwa Spika, TRA imeunda timu maalum kwa ajili ya kuharakisha kutolewa uamuzi wa pingamizi za kodi ndani ya miezi 3. Hadi kufikia Machi 2021, jumla ya pingamizi sitini na nane (68) zimekamilishwa na jumla ya fedha kwa kesi hizo ni TZS 8.25 bilioni, ambapo TZS 6.1 bilioni wahusika wamekata rufaa na TZS 2.15 bilioni zimekusanywa.

iii. Kuwajengea uwezo wafanyakazi;

56. Mheshimiwa Spika, Jumla ya wafanyakazi 65 wa TRA wamejengewa uwezo katika mafunzo ya muda mfupi katika kada ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia, ukusanyaji wa madeni, upelelezi na uchunguzi wa kodi, usimamizi wa sheria za kodi, uongozi na utawala.

Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB)

iv. Kuondoa tofauti ya kodi kwa Mafuta ya "Bunker";

57. Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza utaratibu wa kulipisha Mafuta yote ya dizeli yanayoingizwa nchini kwa kiwango sawa na watumiaji wa vyombo vya baharini vilivyosajiliwa Zanzibar badala ya kuwa na kiwango maalum kwa mafuta ya bunker. Hatua hiyo imetokana na udanganyifu unaofanywa na baadhi ya wafanyabiashara wasiokuwa waaminifu kwa mafuta yanayotumika katika mambo mengine kutajwa pia kama "bunker". Hadi kufikia Machi jumla ya TZS 164 milioni zimekusanywa kutokana na hatua hii.

v. Kuanza rasmi Matumizi ya Mashine za Kielektroniki za Utoaji wa Risiti (VFD's);

58. Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mapato Zanzibar imeendelea na zoezi la kuwafungia wafanyabiashara mashine za VFDs kwa majaribio, ambapo jumla ya machine 154 - Unguja na mashine 45 - Pemba zimefungwa. Aidha, katika kipindi hicho cha majaribio mfumo ulionesha baadhi ya dosari, na sasa dosari hizo zinafanyiwa kazi. Mfumo huo unatarajiwa kuanza kazi rasmi mwaka wa fedha 2021/2022.

vi. Kuendelea Kuwatambua na Kuwagawa Walipakodi katika Mfumo wa Maeneo;

59. Mheshimiwa Spika, ZRB inaendelea na utaratibu wa kuwatambua na Kuwagawa Walipakodi katika Mfumo wa Maeneo (Block Management System), ambapo jumla vibati 320 vya utambuzi vyenye taarifa za walipakodi vimebandikwa katika eneo la Wara - Pemba; maeneo hayo ni Machomane, Wawi, Mkoroshoni na Gombani. Hadi kufikia machi 2021, jumla ya walipakodi wapya 38 wametambuliwa na kuingizwa katika wigo wa kodi.

vii. Kutoa Elimu kwa Walipakodi na Kuwajengea Uwezo Wafanyakazi;

60. **Mheshimiwa Spika,** TRA na ZRB zimeendelea kutoa elimu kwa walipakodi ambapo jumla ya Mikutano 22 imefanyika Unguja na Pemba kwa Wahasibu, Wakandarasi, Washauri wa kodi, Wafanyabiashara na Waandishi wa habari, pamoja na vipindi 47 vya TV na Radio, matangazo 30 pamoja na makala 5.

61. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Kuwajengea Uwezo Wafanyakazi, jumla ya wafanyakazi 152 wamejengewa uwezo katika fani ya "Transfer Pricing" (International Taxation), "Excise Duty framework", "Tax Investigations Skills", "Financial Risks Management", "Statistical Analysis for Researchers", pamoja na "Monitoring and Evaluation Framework".

A. Makadirio ya Matumizi

62. **Mheshimiwa Spika,** Serikali ilipanga kutumia TZS 1,579.2 bilioni ambapo TZS 969.3 bilioni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na TZS 609.9 bilioni ni kwa ajili ya matumizi ya miradi ya maendeleo.

B. Utekelezaji Halisi wa Matumizi ya Serikali kwa kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021

63. **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi hicho cha Mapitio cha Julai-Machi 2020/2021, Jumla ya Matumizi halisi yalifikia TZS 723.3 bilioni sawa na asilimia 62.1 ya makisio ya TZS 1,167 bilioni ya lengo la kipindi hicho na asilimia 45.8 kwa makadirio ya mwaka.

64. **Mheshimiwa Spika,** Kati ya matumizi hayo TZS 550.1 bilioni zilitumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 72 ya makisio ya TZS 763.7 bilioni ya kipindi hicho na asilimia 57.4 ya makadirio ya mwaka. Aidha, TZS 173.2 bilioni zilitumika Kwa Kazi za Maendeleo sawa na asilimia 42.9 ya makisio ya TZS 403.3 bilioni ya kipindi hicho na asilimia 27 ya makadirio ya mwaka.

65. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Fedha zilizotumika kwa Kazi za Maendeleo, TZS 53.5 bilioni zinatokana na fedha za Serikali ambazo ni sawa na asilimia 56.7 ya Makisio ya TZS 94.3 bilioni kwa kipindi hicho na asilimia 27.1 ya makadirio ya mwaka na TZS 119.7 bilioni zinatokana na Washirika wa Maendeleo sawa na asilimia 39 ya makadirio ya TZS 306.0 bilioni kwa kipindi hicho na asilimia 29 ya makadirio ya mwaka.

66. **Mheshimiwa Spika,** Kiwango hicho cha utekelezaji wa miradi kwa upande wa Washirika wa Maendeleo kinatokana na sababu mbalimbali zikiwemo kutokamilika taratibu za manunuzi kwa baadhi ya miradi na kuwepo kwa Maradhi ya Korona. Hali hii, imepelekea kutoingiziwa kiasi chochote cha Fedha kwa baadhi ya miradi mikubwa kwa zaidi ya TZS 194 bilioni zilizokadiriwa, ikiwemo Big Z, Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Abeid Aman Karume Terminal III na ZEST, sambamba na upokeaji mdogo wa fedha kwa baadhi ya miradi.

I. Matumizi ya Huduma za Mfuko Mkuu

67. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha miezi tisa jumla ya TZS 136.4 bilioni, sawa na asilimia 75 ya makadirio ya kipindi hicho ya TZS 182.1 bilioni zilitumika kwa huduma mbalimbali kupitia Mfuko Mkuu wa Serikali. Matumizi hayo yameelekezwa katika mambo yafuatayo:
    a. Malipo ya Kiinua Mgongo TZS 15.8 bilioni kwa wastaafu 885 na Pencheni ya TZS 22.8 bilioni kwa wastaafu 14,084 kwa mwezi;
    b. Malipo ya Mikopo ya ndani na Riba ni TZS 13.5 bilioni;
    c. Matumizi mengine ya Serikali kupitia Mfuko Mkuu TZS 84.3 bilioni.

II. Matumizi ya Mfuko wa Miundombinu

68. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa matumizi ya Mfuko wa Miundombinu jumla ya TZS 44.2 bilioni zilipangwa kutumika kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa Miradi kumi na tano (15) kwa mwaka. Kwa kipindi cha miezi tisa, jumla ya TZS 14.1 bilioni zimetumika kutoka Mfuko wa Miundombinu kwa kugharamia miradi minane (8) sawa na asilimia 32 ya makadirio ya mwaka.

III. Deni la Taifa

69. **Mheshimiwa Spika,** Deni la Taifa linajumuisha Deni la Nje na Ndani linalosimamiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

70. **Mheshimiwa Spika,** Deni la Taifa hadi kufikia Machi 2021, lilikuwa TZS 894.6 bilioni, Deni hilo limeongezeka kwa TZS 77.9 bilioni sawa na asilimia 9.5 ikilinganishwa na Deni lililoripotiwa katika mwezi Machi 2020, ambalo lilikuwa TZS 816.6 bilioni.

i. Deni la Nje

71. **Mheshimiwa Spika,** Deni la Nje hadi kufikia Machi 2021, lilikuwa TZS 688.4 bilioni ambalo ni ziada kwa TZS 27.7 bilioni sawa na asilimia 4.19 ikilinganishwa na deni lililoripotiwa katika mwezi Machi 2020, ambalo lilikuwa TZS 660.7 bilioni. Kati ya deni hilo la TZS 660.2 bilioni sawa na asilimia 95.76 linadhaminiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na TZS 28.3 bilioni sawa na asilimia 4.24 ni Deni la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

ii. Deni la Ndani

72. **Mheshimiwa Spika,** Deni la Ndani hadi kufikia Machi 2021 ni TZS 206.2 bilioni ambalo limeongezeka kwa TZS 50.5 bilioni sawa na ongezeko la asilimia 32.3 ikilinganishwa na Deni lililorikodiwa

katika mwezi Machi 2020, ambalo lilikuwa TZS 155.7 bilioni. Sababu ya kuongezeka kwa Deni hilo ni kupokea mikopo mipya ya hatifungani za muda mrefu pamoja na kupokea sehemu ya mkopo wa ZSSF.

iii. Uhimilivu wa Deni

73. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia tarehe 31 Machi 2021, uwiano wa Deni na Pato la Taifa (GDP) ni asilimia 22, hii inaonesha kuwa Deni bado ni himilivu. Hali hiyo inaonyesha kuwa Serikali bado ina uwezo wa kukopa kwa ajili ya kutekeleza shughuli za maendeleo nchini.

V. MATARAJIO YA MAPATO NA MATUMIZI JULAI 2020 HADI JUNI 2021

A. Matarajio ya Mapato Julai 2020-Juni 2021

74. **Mheshimiwa Spika,** Matarajio ya Serikali ifikapo June 30 mwaka 2021, mapato ya Serikali yatafikia jumla ya TZS 1,024.9 bilioni sawa na asilimia 64.9 ya makadirio ya mwaka, ambapo Mapato ya ndani yanatarajiwa kufikia jumla ya TZS 769.7 bilioni sawa na asilimia 73.3 ya makadirio ya awali. Kiwango hicho kinaonesha upungufu wa asilimia 2.2 ikilinganishwa na ukusanyaji wa mapato kwa mwaka uliopita ya TZS 787.2 bilioni.

75. **Mheshimiwa Spika,** Mapato ya kodi yanatarajiwa kufikia TZS 655.2 bilioni, sawa na asilimia 71 ya bajeti ya TZS 921.3 bilioni, ambapo ni sawa na upungufu wa asilimia 3 ikilinganishwa na ukusanyaji wa mapato ya TZS 675.2 bilioni kwa mwaka wa fedha uliopita 2019/20 kwa mchanganuo ufuatao:

i. Kati ya kiasi hicho, matarajio ni kuwa Mamlaka ya Mapato Tanzania - Zanzibar (TRA) kukusanya TZS 298.2 bilioni sawa na asilimia 77.8 ya Makadirio ya TZS 383.5 bilioni. Mapato

hayo yanaonesha ukuaji wa asilimia 14 ikilinganishwa na mapato ya TZS 279.4 bilioni yaliyokusanywa kwa mwaka wa fedha uliopita 2019/2020.

ii. Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) inatarajiwa kukusanya TZS 335.9 bilioni sawa na asilimia 65 ya Makadirio ya TZS 516.7 bilioni ambapo ni sawa na upungufu wa asilimia 16 ikilinganishwa na ukusanyaji wa mapato ya TZS 374.8 bilioni kwa mwaka wa fedha uliopita 2019/2020.

iii. Kodi ya Mapato kutoka Serikali ya Jamuhuri ya Muungano inatarajiwa kufikia TZS 21.0 bilioni sawa na asilimia 100 ya lengo.

76. **Mheshimiwa Spika,** Mapato yasiyokuwa ya kodi yanatarajiwa kufikia TZS 114.6 bilioni sawa na asilimia 89, ambapo ni sawa na ukuaji wa asilimia 2 ikilinganishwa na ukusanyaji wa mapato wa TZS 112.0 bilioni kwa mwaka wa fedha uliopita 2019/2020 kwa mchanganuo ufuatao;

i. Mapato ya Wizara yanategemewa kufikia TZS 98.8 bilioni sawa na asilimia 94 ya makadirio ya mwaka ya TZS 104.7 bilioni;

ii. Gawio la Mashirika ya Serikali linatarajiwa kufikia TZS 9.04 bilioni sawa na asilimia 86 ya makadirio ya mwaka ya TZS 10.5 bilioni.

iii. Gawio la Benki Kuu ya Tanzania, linatarajiwa kufikia TZS 6.7 bilioni sawa na asilimia 49.6 ya makadirio ya mwaka ya TZS 13.5 bilioni.

77. **Mheshimiwa Spika,** Matarajio ya mapato ya Mfuko wa Miundombinu ni kufikia TZS 37.7 bilioni sawa na asilimia 85 ya makadirio ya Bajeti, ambapo TRA inatarajiwa kukusanya TZS 11.1 bilioni na ZRB inatarajiwa kukusanya TZS 26.5 bilioni.

78. **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa mapato kutoka kwa Washirika wa Maendeleo yanatarajiwa kufikia TZS 154.6 bilioni sawa na asilimia 36.4 ya makadirio ambapo Ruzuku ni TZS 44.6 bilioni na mikopo ni TZS 110 bilioni.

79. **Mheshimiwa Spika,** Mkopo wa ndani matarajio ni kufikia TZS 101.2 bilioni sawa na asilimia 224.9 ya makadirio. Kiwango hicho kikubwa cha madeni ya ndani kinatokana na ziada ya nakisi ya Bajeti kugharamiwa na bakaa la deni la nyuma (roll over) lililo haulishiwa katika mwaka huu wa Fedha.

B. Matarajio ya Matumizi Julai 2020-Juni 2021

80. **Mheshimiwa Spika,** Matumizi ya Serikali hadi kumalizika kwa mwaka wa Fedha 2020/2021 yanatarajiwa kufikia TZS 1,024.9 bilioni sawa na asilimia 64.9 ya bajeti ya mwaka ya TZS 1,579.2 bilioni, ambapo jumla ya TZS 733.6 bilioni zitatumika kwa matumizi ya Kazi za Kawaida sawa na asilimia 75.7 na TZS 291.3 bilioni kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo sawa na asilimia 47.8 ya makadirio ya awali kwa Mchanganuo ufuatao:

i. Matumizi ya Mishahara yanatarajiwa kufikia TZS 408.3 bilioni ambapo TZS 276.0 bilioni kwa Wizara na Taasisi zenye Mafungu, sawa na asilimia 87.1 ya bajeti ya mwaka na TZS 132.3 bilioni zimetumika kulipa mishahara ya Taasisi zinazopokea Ruzuku, sawa na asilimia 106.9 ya bajeti ya mwaka. Kutofikiwa matarajio ya matumizi ya mishahara ya Mafungu kunatokana na matarajio ya bakaa ya kifungu cha marekebisho ya mshahara (salary adjustment) zilizopangwa kulipwa kwa ajili ya marekebisho mbalimbali ya mshahara;

ii. Matumizi Mengineyo ya kuendeshea Ofisi, jumla ya TZS 157.4 bilioni ambapo kwa Wizara na Taasisi zenye Mafungu matarajio ni kutumia TZS 85.6 bilioni sawa na asilimia 46.9 ya makadirio ya mwaka, wakati kwa Taasisi zinazopokea Ruzuku yanatarajiwa kufikia TZS 71.8 bilioni, sawa asilimia 66.4 ya makadirio ya mwaka. Matarajio hayo yanatokana na kuendelea kuwepo kwa changamoto ya makusanyo kutokana na athari za COVID 19, na Maamuzi ya Serikali kuelekeza zaidi matumizi katika Miradi ya Maendeleo;

iii. Matumizi ya Mfuko Mkuu wa Serikali yanatarajiwa kufikia TZS

167.9 bilioni, sawa na asilimia 70.6 ya makadirio ya mwaka mzima;

iv. Matumizi ya Kazi za Maendeleo kwa fedha za ndani yanatarajiwa kufikia TZS 137.3 bilioni sawa na asilimia 69.6 ya makadirio ya mwaka; na

v. Mikopo na Ruzuku kutoka kwa Washirika wa Maendeleo Serikali inatarajia kupokea TZS 154.0 bilioni, sawa na asilimia 37.3 ya makadirio ya mwaka.

VI. SERA ZA BAJETI NA MIKAKATI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

81. Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka wa Fedha 2021/2022 Serikali imedhamiria kusimamia utekelezaji wa ***"Mipango na Bajeti inayoakisi Uchumi wa Buluu kwa Maendeleo ya Zanzibar na Watu wake"*** kwa kuelekeza nguvu zake katika maeneo yafuatayo:

a. Utekelezaji wa ilani ya CCM ya mwaka 2020-2025 kwa kuandaa mkakati wa kufanikisha na kuhakikisha malengo yanatekelezwa kwa ufanisi na kuleta tija kwa walengwa;

b. Kuimarisha Maendeleo ya rasilimali watu na huduma za kijamii kwa kusaidia Sekta binafsi kuwawekea mazingira rafiki na utaratibu mzuri wa mazingira ya kazi kwa lengo la kukuza ajira;

c. Kuelekeza Rasilimali fedha katika maeneo ya kipaumbele yatakayochochea ajira rasmi na zisizo rasmi;

d. Kuimarisha Mageuzi ya Uchumi katika maeneo ya uzalishaji viwandani, utalii endelevu na kilimo cha kisasa;

e. Kustawisha sekta ya Uchumi wa Buluu ambayo ni moja katika sekta kiongozi katika uchumi wa Zanzibar kwa kurahisisha utekelezaji wa Mpango Mkuu wa matumizi ya Rasilimali za Bahari na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi asilia;

f. Kujenga Ushiriki mpana wa sekta binafsi kwa kuweka misingi imara ya mashirikiano katika miradi ya kimkakati;

g. Kusimamia utendaji wa Serikali, katika eneo la nidhamu, uwajibikaji, sambamba na ubunifu wa kazi ili kuondokana na kufanya kazi kwa mazowea;

h. Kuimarisha taratibu za Bajeti na uandaaji wa mipango kwa kuboresha mifumo ya ndani ili iende sambamba na utekelezaji wa malengo ya kitaifa na kimataifa kwa kuweka ukadiriaji bora wa mapato na usimamizi mzuri wa matumizi ikiwa pamoja na;

i. Kuchukua juhudi za makusudi katika kuimarisha suala la mifumo ya Serikali ili kuweza kupunguza upotevu wa Fedha za umma na Kudhibiti matumizi yasiyokuwa na Tija kwa kuhimiza matumizi sahihi ya mifumo ya Kielektroniki;

ii. Kufanya Mageuzi ya mfumo wa Bajeti na Malipo kwa kuandaa utaratibu wa kuunganisha Mipango, Bajeti na Matumizi katika Mfumo mmoja wa Bajeti na Malipo ya Serikali;

iii. Kuanzisha utaratibu wa kufanya tathmini ya matumizi ya Serikali na Usimamizi wa Fedha (Public Expenditure Review);

iv. Kuanza mchakato wa kuaandaa Sheria ya Bajeti (Budget Act and Budget Manual)

v. Kuanzisha mfumo wa Ununuzi utakaounganisha hatua zote za malipo kwa elektroniki

vi. Kuwajengea uwezo wataalamu wa ndani kwenye eneo la usalama wa mifumo;

VII. MAPENDEKEZO YA HATUA ZA KUIMARISHA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

82. Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikichukua hatua kadhaa za kuweka mfumo wa kodi uliotulivu na wenye kutabirika, kushajihisha ulipaji wa Kodi kwa hiari, kukuza ajira na kuongeza mapato ya Serikali na hivyo kuchochea kasi ya ukuaji wa Uchumi hususan katika Sekta ya Viwanda. Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali haipendekezi kupandisha kodi yoyote katika vyanzo vyake vya

ndani, badala yake itaendelea kuchukua hatua kadhaa za kuimarisha usimamizi na ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

83. Mheshimiwa Spika, Hatua hizo zinazopendekezwa kuchukuliwa na Serikali ni zile zinazohusu marekebisho ya Sheria pamoja na zinazohusu kuimarisha Usimamizi na Utawala wa Kodi.

A. Hatua zinazohusu Marekebisho ya Sheria

i. Kampuni kutoka Tanzania Bara Kuchangia katika Uchumi wa Zanzibar kwa Kulipa Kodi ya Mapato Zanzibar.

84. Mheshimiwa Spika, Serikali inakusudia kufanya marekebisho katika Sheria ya Kampuni Namba 15 ya mwaka 2013 kwa lengo la kuwawezesha Kampuni kutoka Tanzania Bara kuchangia katika uchumi wa Zanzibar kwa kulipa Kodi ya Mapato Zanzibar ambapo watakuwa wanafanya biashara zao. Hatua hii inatarajiwa kukusanya jumla TZS 2.7 bilioni.

ii. Kuondoa ulipaji VAT Mara Mbili baina ya Tanzania Bara na Zanzibar

85. Mheshimiwa Spika, Kwa muda mrefu mfumo wa VAT kwa Zanzibar na Tanzania Bara umebainika kuwa na changamoto kadhaa ikiwemo ulipaji VAT mara mbili kwa bidhaa zinazoingia Zanzibar kutoka Tanzania Bara. Baada ya mashauriano baina ya Serikali mbili (SMZ na SMT) Serikali inapendekeza kufanya Marekebisho ya Sheria ya Ongezeko la Thamani Namba 4 ya mwaka 1998 kufuta kodi ya VAT wakati wa kuingiza bidhaa Zanzibar kutoka Tanzania Bara. Hata hivyo, fursa hii ni kwa wale ambao watawasilisha kwa ZRB risiti na stakabadhi za bidhaa zao walizonunulia Tanzania Bara. Hatua hii inatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha TZS 15.0 bilioni.

iii. Kufuta Viwango Maalum (specific rates) vya Ushuru wa Hotel na Kuweka Utaratibu wa Utozaji Ushuru wa Hoteli kwa Nyumba za Kulala Wageni Zinazotumia Jukwaa la "Airbnb";

86. Mheshimiwa Spika, Kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wafanyabiashara waliosajiliwa chini ya Sheria ya Ushuru wa Hoteli juu ya uwepo wa:

i. Wananchi na wafanyabiashara wanaokodisha nyumba zao binafsi kwa utaratibu wa jukwaa (Platform) la "Airbnb" na majukwaa mengine yanayofanana nayo; na
ii. Utaratibu wa kutoza kodi kwa kiwango maalum (specific rates).

87. Mheshimiwa Spika, Kwa lengo la kuondoa changamoto hizo pamoja na kuleta usawa katika kutoza Ushuru wa Hoteli, Serikali inapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Hoteli Namba 1 ya mwaka 1995 kama ifuatavyo;-

(a) Kufuta viwango maalum (specific rates) vya kutozea Ushuru wa Hoteli; na
(b) Kuweka kiwango cha asilimia 15 ya pango (rent) kwa wanaokodisha nyumba zao kwa utaratibu wa jukwaa (Platform) la "Airbnb" na majukwaa mengine yanayofanana nayo.

iv. Kupunguza Kiwango cha VAT na Ushuru wa Forodha Kushajihisha Uwekezaji katika Uzalishaji wa Viwanda vya Nguo;

88. Mheshimiwa Spika, Kwa lengo la kushajihisha uwekezaji katika sekta ya viwanda vya uzalishaji nguo, Serikali inapendekeza kupunguza kiwango cha VAT na ushuru wa forodha ili kutoa unafuu maalum wa kodi kwa wazalishaji wa nguo kama ifuatavyo: -

a) Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye vifaa vyenye HS Code 8444.00.00, 8445.11.00, 8445.12.00, 8445.13.00, 8445.19.00, 8445.20.00, 8445.30.00, 8445.40.00, 8445.90.00, 8446.10.00, 8446.21.00, 8446.29.00, 8446.30.00, 84.47, 8448.11.00, 8448.19.00, 8449.00.00, 8451.40.00 au 8451.50.00.

b) Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 25 hadi asilimia 10 kwa mwaka mmoja kwa utaratibu wa "duty remission" kwenye malighafi zenye HS Code 5407.71.00, 3402.90.00, 3506.91.00, 3208.20.00 na 3208.90.00 zinazotumika kwenye kutengeneza nguo.

c) Kupunguza Ushuru wa Forodha kutoka asilimia 10 hadi asilimia 0 kwa mwaka mmoja kwa utaratibu wa "duty remission" kwenye malighafi yenye HS Code 5402.33.00 inayotumika kwenye kutengeneza nguo.

v. Kuanza Kukusanya Mapato ya Serikali kwa Kutumia Mfumo Mpya wa Kielektroniki Ujulikanao kama "ZanMalipo";

89. Mheshimiwa Spika, Dhamira ya muda mrefu ya Serikali ni kuanza kukusanya mapato yote ya kodi na yasiokuwa ya kodi kwa kutumia mfumo wa kielektroniki kwa lengo la kulinda mapato ya Serikali na kurahisisha ukusanyaji wake. Serikali inapendekeza kufanya Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Namba 12 ya mwaka 2016 kuzitaka Taasisi zote za Serikali kuanza kutumia mfumo wa kielektroniki ujulikanao kama "ZanMalipo". Lengo la mfumo huu ni kupunguza mianya ya upotevu wa mapato, kupunguza gharama za ukusanyaji pamoja na kuweka uwazi katika ulipaji wa bidhaa na huduma za Serikali. Hatua hii inatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha TZS 7.5 bilioni.

vi. Kudhibiti Ufungaji wa Biashara na Hesabu za Benki za Walipakodi;

90. Mheshimiwa Spika, Kumekuwa na malalamiko ya walipakodi juu ya usumbufu wanaoupata kwa kufungiwa biashara zao na hesabu

zao za benki na Bodi ya Mapato Zanzibar. Katika kurekebisha kasoro hiyo Serikali inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Utaratibu na Usimamizi wa Kodi Namba 7 ya mwaka 2009 kuzuia ufungaji wa biashara na hesabu za benki za walipakodi, isipokuwa kwa idhini ya Kamishna kwa maandishi.

vii. Kuweka Adhabu kwa Wanufaika wa Misamaha ya Kodi, Watakapoitumia Kinyume na Malengo;

91. **Mheshimiwa Spika,** Kuna baadhi ya wanufaika wa misamaha ya kodi ambao hutumia misamaha wanayopewa kinyume na malengo yaliyowekwa na Serikali. Hivyo, kwa lengo la kuongeza usimamizi na udhibiti wa misamaha Serikali inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Utaratibu na Usimamizi wa Kodi Namba 7 ya mwaka 2009 kwa kuweka adhabu kali kwa wanufaika hao ikiwa ni pamoja na kulipa kodi iliyosamehewa, kulipa adhabu ya asilimia 50 ya kodi stahiki na kuzuiliwa kupewa msamaha siku za usoni.

viii. Kutoa unafuu wa Ushuru wa Stempu kwa Wafanyabiashara Wadogo na Wakati

92. **Mheshimiwa Spika,** Kumekuwa na malalamiko ya kutozwa viwango vikubwa vya Ushuru wa Stempu kwa Wafanyabashara Wadogo na Wakati. Kwa lengo la kuendelea kuwapunguzia mzigo wa kodi na kuwaongezea kipato wafanyabiashara hao, Serikali inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Stempu Namba 7 ya mwaka 2017 kama ifuatavyo: -

a) kusamehe Ushuru wa Stempu kwenye mauzo ghafi yasiozidi TZS 5.0 milioni kwa wenye vitambulisho vya wajasiriamali vinavyotolewa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
b) kupunguza viwango maalum kutoka TZS 200,000 hadi TZS 100,000 kwa mwaka na kutoka TZS 732,500 hadi TZS 200,000 kwa mwaka;
c) kupunguza kiwango cha Ushuru wa Stempu kutoka asilimia

3 hadi asilimia 2 kwenye mauzo ghafi yanayozidi TZS 15.0 milioni. Jadweli namba 1 linafafanua zaidi

Jadweli Nam 1: Mapendekezo ya Viwango vya ushuru wa stempu .

No.	Mauzo kwa TZS	Kiwango kwa Mwaka 'TZS'
1.	Mauzo yasiozidi TZS 5,000,000 kwa mwaka	NIL
2.	Mauzo yanayozidi TZS 5,000,000 lakini hayazidi TZS 10,000,000	100,000
3.	Mauzo yanayozidi TZS 10,000,000 lakini hayazidi TZS 15,000,000	200,000
4.	Mauzo yanayozidi TZS 15,000,000	2% ya mauzo

ix. Kupunguza Viwango vya Kodi ya Mapato (Income Tax) kwa Wafanyabiashara Binafsi na Wafanyakazi.

93. Mheshimiwa Spika, Kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu kutoka kwa wafanyabiashara binafsi na wafanyakazi waliopo Zanzibar kuhusu uwepo wa viwango vikubwa vya kutoza Kodi ya Mapato ukilinganisha na viwango vya Tanzania Bara. Kwa lengo la kurekebisha kasoro hiyo na kupunguza mzigo wa kodi kwa wafanyakazi na wafanyabiashara binafsi, Serikali inapendekeza kufanyika kwa marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Mapato Namba 11 ya 2004 kufuta viwango vya sasa kama inavyooneshwa katika Jadweli Namba 2 na kuweka viwango vipya kama inavyooneshwa katika jadweli namba 3.

Jadweli Nam 2: Viwango vya Sasa vya Kodi ya Mapato kwa Wafanyabiashara Binafsi na Wafanyakazi

Mapato kwa Mwezi	Kiwango cha Kodi
Mapato yasiozidi TZS 180,000/-	Hakuna kodi
Mapato yanayozidi TZS 180,000/- lakini hayazidi TZS 360,000/-	9% ya mapato yanayozidi Shs 180,000/-
Mapato yanayozidi TZS 360,000/- lakini hayazidi TZS 540,000/-	TZS 16,200 + 20% ya mapato yanayozidi TZS 360,000/-
Mapato yanayozidi TZS 540,000/- lakini hayazidi TZS 720,000/-	TZS 52,200 + 25% ya mapato yanayozidi TZS 540,000/-
Mapato yanayozidi TZS 720,000/-	TZS 97,200 + 30% ya mapato yanayozidi TZS 720,000/-

Jadweli Nam 3: Mapendekezo ya Viwango vya Kodi ya Mapato kwa Wafanyabiashara Binafsi na Wafanyakazi

Mapato kwa Mwezi	Kiwango cha Kodi
Mapato yasiozidi TZS 270,000/-	Hakuna kodi
Mapato yanayozidi TZS 270,000/- lakini hayazidi TZS 520,000/-	8% ya mapato yanayozidi TZS 270,000/-
Mapato yanayozidi TZS 520,000/- lakini hayazidi TZS 760,000/-	TZS 20,000 + 20% ya mapato yanayozidi TZS 520,000/-
Mapato yanayozidi TZS 760,000/- lakini hayazidi TZS 1,000,000/-	TZS 68,000 + 25% ya mapato yanayozidi TZS 760,000/-
Mapato yanayozidi TZS 1,000,000/-	TZS 128,000 + 30% ya mapato yanayozidi TZS 1,000,000/-

x. Kuongeza Kiwango cha Adhabu kwa Wasiotoa Risiti.

94. Mheshimiwa Spika, Kwa lengo la kulinda upotevu wa mapato ya Serikali kutokana na kutokutoa risiti, Serikali inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Utaratibu na Usimamizi wa Kodi Namba 7 ya mwaka 2009 kwa kuweka adhabu ya TZS 2 milioni kwa kila muamala kwa wafanyabiashara ambao hawatoi risiti.

xi. Kuongeza Muda kwa Ankara ya Kodi Kuruhusiwa Kupunguza VAT Kutokana na Manunuzi.

95. Mheshimiwa Spika, Ili kuwapa muda wa kutosha wafanyabiashara waliosajiliwa katika VAT kudai marejesho ya VAT kutokana na

manunuzi, Serikali inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Ongezeko la Thamani Namba 4 ya mwaka 1998 kwa kuongeza muda kwa Ankara ya Kodi kuruhusiwa kupunguza VAT kutokana na manunuzi, kutoka miezi 3 hadi 6.

xii. Kuweka Muda Maalum kwa Bodi na Baraza la Rufaa za Kodi kutoa Maamuzi ya Rufaa za Kodi.

96. Mheshimiwa Spika, Kutokana na ucheleweshaji wa utoaji wa maamuzi ya pingamizi za kodi katika Bodi na Baraza la Rufaa za kodi, Serikali inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Rufaa za Kodi Zanzibar namba 1 ya mwaka 2006 ili maamuzi ya pingamizi hizo yatolewe ndani ya siku 90 baada ya pingamizi husika kusikilizwa kwa lengo la kuharakisha utoaji wa maamuzi hayo.

xiii. Kufuta Tozo ya Biashara (Trade Levy)

97. Mheshimiwa Spika, Kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu kutoka kwa wafanyabiashara juu ya utozaji wa kodi nyingi ikiwemo Tozo ya Biashara na hivyo kuongeza gharama za kuendesha biashara. Serikali inapendekeza kufanya marekebisho ya Kanuni za Ada na tozo ya mwaka 2015 kufuta Tozo la Biashara.

xiv. Kuandaa utaratibu wa Utozaji wa Ada ya Uhifadhi wa Mazingira katika Uhamishaji wa Mafuta kwa Njia ya Meli "ship to ship".

98. Mheshimiwa Spika, Kumekuwa na ongezeko la biashara ya Uhamishaji wa mafuta kutoka kwenye meli kubwa kwenda kwenye meli ndogo "ship to ship" katika Bahari ya Zanzibar na hivyo kuhatarisha mazingira ya Bahari. Ili kukabiliana na hali hiyo, Serikali inapendekeza kuanza maandalizi ya utozaji wa Ada ya Uhifadhi wa Mazingira.

xv. Kuondoa Sharti la Malipo ya Awali ya Asilimia 25 ya Kodi Wakati wa Kulipa Kodi kwa Utaratibu wa Awamu.

99. Mheshimiwa Spika, Walipakodi wanashidwa kusawazisha malipo yao ya kodi kwa Bodi ya Mapato Zanzibar kutokana na kuwepo kwa sharti la kisheria la kulipa asilimia 25 ya kodi ili kuruhusiwa kulipa kodi kwa utaratibu wa awamu (installment payments). Serikali inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Utaratibu na Usimamizi wa Kodi Namba 7 ya mwaka 2009 kufuta sharti hilo.

xvi. Kuondoa VAT kwa Bidhaa za Mafuta ya Kupikia, Sukari, Mabati, Nondo na Saruji.

100. Mheshimiwa Spika, Kwa lengo la kuleta unafuu wa kodi kwa wananchi pamoja na kuimarisha ustawi wa jamii, Serikali inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Ongezeko la thamani Namba 4 ya mwaka 1998 kuondoa VAT kwa bidhaa za Mafuta ya kupikia, Sukari, Mabati, Nondo na Saruji.

xvii. Kuzuia Uhaulishaji wa Ardhi, Majengo na Hisa Bila ya Cheti cha Ruhusa ya Kodi (Tax Clearance Certificate).

101. Mheshimiwa Spika, Katika kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato kutokana na uhaulishaji wa Ardhi, Majengo na Hisa, Serikali inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Uhaulishaji wa Ardhi Namba 8 ya mwaka 1994 na Sheria ya Kampuni Namba 15 2013 kuweka sharti la kuwasilisha Cheti cha Ruhusa ya Kodi (Tax Clearance) wakati wa uhaulishaji kabla ya kubadilisha umiliki wa Ardhi, Majengo na Hisa.

B. Hatua za Kuimarisha Usimamizi na Utawala wa Kodi

i. Kuunganisha Mfumo wa Tehama wa Bodi ya Mapato Zanzibar na Mamlaka ya Mapato Tanzania.

102. Mheshimiwa Spika, Serikali imepanga kuunganisha mfumo wa ukusanyaji wa kodi wa Bodi ya Mapato Zanzibar na Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa lengo la kurahisisha kuwatambua walipakodi, kubadilishana taarifa za kodi na ufuatiliaji wa madeni ya kodi.

ii. Kuwatambua Wafanyabiashara wa Mtandaoni

103. Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mapato Zanzibar na Mamlaka ya Mapato Tanzania zinakusudia kuwatambua wanafanyabiashara wa mtandaoni kwa lengo la kuwasaidia kutimiza wajibu wao wa kulipa kodi kwa urahisi na hivyo kuongeza wigo wa kodi.

iii. Kuendeleza Mfumo wa Kuwatambua Walipakodi Kimaeneo (Block Management System)

104. Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mapato Zanzibar na Mamlaka ya Mapato Tanzania zitaendelea na zoezi la kuwatambua walipakodi kimaeneo (Block Management System) kwa lengo la kuwaingiza katika mfumo wa kodi.

iv. Kuendelea na Ukaguzi wa Kodi katika Taasisi za Fedha na Kampuni za Mawasiliano

105. Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mapato Zanzibar na Mamlaka ya Mapato Tanzania zitaendelea kushirikiana kufanya Ukaguzi wa Kodi kwa lengo kuhakikisha kwamba Kodi stahiki inalipwa.

v. Kupata Taarifa za Kodi Kutoka Chanzo cha Tatu.

106. Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mapato Zanzibar inakusudia kuingia Makubaliano na Taasisi za Serikali kwa lengo la kurahisisha

upatikanaji wa taarifa za kodi kutoka chanzo cha tatu na kuzifanyia uchambuzi kupitia kitengo cha "Business Intelligence Unit" ili kuongeza wigo wa kodi.

vi. Kugomboa Madeni ya Kodi

107. Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mapato Zanzibar na Mamlaka ya Mapato Tanzania zitaendelea na zoezi la kufanya uhakiki wa madeni ya kodi, ukaguzi na upelelezi wa kodi pamoja na kuchukua hatua stahiki za kisheria katika kuhakikisha kwamba madeni ya kodi yanalipwa.

vii. Kuanza kutoza Kodi ya Majengo (Property Tax)

108. Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mapato Zanzibar inatarajia kuanza ukusanyaji wa kodi ya majengo baada ya kukamilika kwa mfumo wa ukusanyaji wa taarifa za majengo pamoja na viwango maalum (specific amount) vya kutozea kodi husika. Serikali inapendekeza kuanza kutoza kodi hiyo kwa kiwango cha TZS 10,000 kwa kila nyumba ya kawaida na kiwango cha TZS 50,000 kwa kila ghorofa moja, kwa mwaka.

viii. Kuanzisha Mfumo wa Kielektroniki Utakaowezesha Kupata Taarifa za Wageni Wanaoingia Nchini

109. Mheshimiwa Spika, Kamisheni ya Utalii kwa kushirikiana na Bodi ya Mapato Zanzibar na Mamlaka ya Mapato Tanzania inatarajia kuanzisha mfumo wa kielektroniki utakaosaidia kujua idadi ya wageni wanaongia nchini, wageni wanaolala katika mahoteli na nyumba za kulala wageni, pamoja na kujua bei halisi wanazolipa kutokana na huduma wanazopata.

ix. Kuanzisha Kanzidata ya Uthaminishaji Bidhaa

110. Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mapato Tanzania inakusudia kuanzisha kanzidata ya uthaminishaji bidhaa zinazoingia nchini

utakaotumika kukokotoa kodi ya Forodha kwa lengo la kuongeza uwazi na ufanisi.

x. Kuongeza Kiwango cha Gawio kutoka Mashirika ya Serikali

111. Mheshimiwa Spika, Kufuatia kuimarika kwa Mashirika ya Serikali kutokana na kuongezeka kwa ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao, Serikali inapendekeza kuongeza kiwango cha Gawio kutoka katika Mashirika ya Serikali kutoka asilimia 20 hadi asilimia 50 kwa lengo la kuchangia katika Bajeti ya Serikali.

VIII. SURA YA BAJETI.

112. Mheshimiwa Spika, Kwa mwaka wa Fedha 2021/2022, Serikali inakadiria kukusanya Mapato na kufanya Matumizi ya Jumla ya TZS 1,845.6 bilioni (zikiwemo TZS 1,829.9 bilioni kwa Serikali Kuu na TZS 15.7 bilioni kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa)

A. Makadirio ya Mapato

a. Mapato ya Ndani

113. Mheshimiwa Spika, Jumla ya TZS 1,134.9 bilioni zimekadiriwa kukusanywa kutoka katika Mapato ya ndani sawa na asilimia 61.5 ya makadirio yote ambayo tunatarajia kuyakusanya kwa mwaka wa fedha 2021/22.

Makadirio ya Ukusanyaji Kitaasisi

114. Mheshimiwa Spika, Kati ya makadirio hayo, mapato yanayotokana na kodi yanatarajiwa kufikia TZS 959.2 bilioni ambapo kati ya fedha hizo:-

i. TZS 413.1 bilioni kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzanian (TRA);
ii. TZS 525.1 bilioni kutoka Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) na
iii. TZS 21 bilioni Mapato ya kodi yatokanayo na wafanyakazi kutoka SMT walioko Zanzibar.

115. Mheshimiwa Spika, Mapato yasiyo ya kodi yamekadiriwa kufikia TZS 175.7 bilioni yanayojumuisha:-
i. TZS 137.3 bilioni, makusanyo ya Mapato ya Mawizara;
ii. TZS 25.7 bilioni, Gawio la Mashirika ya Serikali na
iii. TZS 13.5 bilioni, Gawio kutoka Benki Kuu ya Tanzania.

b. Mikopo ya Ndani na Nje

116. Mheshimiwa Spika, Serikali inatarajia kukopa kutoka Ndani na Nje ili kuziba Nakisi ya Bajeti jumla ya TZS 312 bilioni sawa na asilimia 16.9 ya makadirio ya Bajeti yote kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

c. Ruzuku na Mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo

117. Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa Washirika wa Maendeleo Serikali imekadiria kupokea Jumla ya TZS 383.0 bilioni sawa na asilimia 20.7 ya makadirio ya Bajeti yote zikiwemo: -
i. TZS 204.0 bilioni Mkopo kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo;
ii. TZS 79 bilioni Ruzuku (zikiwemo TZS 65.5 bilioni ruzuku na TZS 13.5 bilioni kutoka Mfuko wa Pamoja na Wafadhili (basket fund);
iii. TZS 20 bilioni na Misaada ya Kibajeti (GBS) na
iv. TZS 80 bilioni Marejesho ya matumizi ya Mkopo zilizotumika katika ujenzi wa Terminal III kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

d. Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa

118. Mheshimiwa Spika, Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kutokana na vyanzo vyake vya ndani yanakadiriwa kukusanywa Jumla ya TZS 15.7 bilioni sawa na asilimia 0.8 ya makadirio ya Bajeti yote.

B. Makadirio ya Matumizi

119. Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa Matumizi, kiasi hicho cha jumla ya TZS 1,845.6 bilioni kwa mwaka wa fedha 2021/2022 (zikiwemo TZS 1,829.9 bilioni kwa Serikali Kuu na TZS 15.7 bilioni kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa) zinatarajiwa kutumika kama ifuatavyo:

a. Matumizi ya Kazi za Kawaida

120. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa Fedha 2021/2022 Matumizi ya kawaida yanakadiriwa kufikia TZS 947.2 bilioni sawa na asilimia 51.3 yakijumuisha: -

i. TZS 364.9 bilioni, Mishahara ya Mafungu;
ii. TZS 76.8 bilioni, Mishahara ya Ruzuku;
iii. TZS 200.2 bilioni, Matumizi ya kuendeshea ofisi ya Mafungu;
iv. TZS 97.5 bilioni, Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida, na
v. TZS 207.7 bilioni, Matumizi ya huduma za Mfuko Mkuu wa Serikali.

b. Matumizi ya Kazi za Maendeleo

121. Mheshimiwa Spika, Makadirio ya matumizi kwa Kazi za Maendeleo ni jumla ya TZS 882.8 bilioni sawa na asilimia 47.8 ya bajeti yote, ikihusisha TZS 606.5 bilioni kutoka Serikalini na TZS 276.3 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ambapo TZS 204.0 bilioni Mkopo, na TZS 72.3 bilioni ni Ruzuku.

122. **Mheshimiwa Spika,** Maelezo ya kina ya Matumizi ya Kazi za Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 nimeshayawasilisha katika Hotuba ya Mpango wa Maendeleo. Naomba kwa uchache niweke msisitizo kwa mambo ya Msingi katika matumizi hayo ya Maendeleo:

i. Kuendelea na matayarisho ya ujenzi wa uwanja wa ndege wa Pemba;
ii. Kuendelea na matayarisho ya ujenzi wa Bandari ya Mangapwani na Mkoani;
iii. Kununua meli nne za uvuvi;
iv. Kuendelea na uwekaji wa miundombinu ya maji katika visima vya Ras el Khaimah;
v. Kuendelea na utekelezaji wa mradi wa Mageuzi ya Sekta ya Nishati (Zanzibar Energy Sector Transformation - ZEST) ambapo inatarajiwa kwa kiasi kikubwa kuwafikisha wananchi wa kipato cha chini kwa kupata huduma ya nishati nafuu;
vi. Kuanza rasmi utekelezaji wa mradi wa Mpango Shirikishi wa Kukuza Uchumi Zanzibar (Boost Inclusive Growth in Zanzibar-Big Z) ambapo jumla ya TZS 5.7 bilioni zimepangwa kutumika katika hatua za awali za maandalizi. Kiujumla mradi huu unatarajiwa kubadilisha taaswira ya mji wa Zanzibar;
vii. Kuanza rasmi uzalishaji wa umeme wa jua na gesi;
viii. Imepanga kutumia jumla ya TZS 73 bilioni kwa ajili ya Uhuishaji na Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji wa Maji Zanzibar;
ix. Kuanza ujenzi wa Chelezo katika eneo la Kibweni;
x. Itaendelea na utekelezaji wa programu ya ajira kwa vijana;
xi. Kuendelea na ujenzi wa Hospitali mpya ya rufaa na kufundishia Binguni;
xii. Kuanza ujenzi wa Hospitali ya Wete;
xiii. Kukuza miundombinu ya elimu na kuandaa mitaala mipya ya elimu ya msingi na maandalizi;
xiv. Kuendeleza ujenzi wa Ofisi za Serikali;
xv. Kutekeleza Programu ya Uimarishaji wa Utoaji Matangazo

ZBC, ambapo jumla ya TZS 19 bilioni zimetengwa kwa ajili ya kuimarisha huduma za mawasiliano Zanzibar;

xvi. Kuendeleza taaluma katika fani mbali mbali ikiwemo mafuta na gesi, uhandisi, huduma za ugani, udaktari na taaluma za sayansi; na

xvii. Kuanzisha na kuimarisha mifumo ya kidijitali ya utendaji kazi kwa ujumla, ukusanyaji mapato, usimamizi wa matumizi, manunuzi na utunzaji. Mradi huu una matumaini makubwa ya kuimarisha ukusanyaji wa mapato na kudhibiti matumizi ya Fedha za Umma.

c. Matumizi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa

123. Mheshimiwa Spika, Matumizi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kutokana na vianzio vyao vya ndani inakadiriwa kufikia TZS 15.7 bilioni sawa na asilimia 0.8 ya makadirio ya Bajeti yote.

124. Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa matumizi ya Mfuko wa Miundombinu jumla ya TZS 46.4 bilioni zimetengwa kwa ajili ya kugharamia miradi maalum ya maendeleo, kwa mwaka 2021/2022 Wizara mbili tu ambazo miradi yake imepangiwa kutumia Fedha hizo kwa lengo la kuongeza Ufanisi wa Matumizi ya mfuko huo. Uchambuzi wa miradi hiyo unaonekana katika **Kiambatanisho**

125. Mheshimiwa Spika, Kwa sura hii ya Bajeti, kunajitokeza taswira ifuatayo:

i. Mapato ya ndani yanayotokana na kodi na yasiyokuwa ya kodi ya TZS 1,134.9 bilioni sawa na asilimia 61.5 ya makadirio ya Bajeti yanaweza kugharamia matumizi yetu yote ya kazi za kawaida ya jumla ya TZS 947.1 bilioni sawa na asilimia 51.3 ya makadirio ya Bajeti.

ii. Kiwango cha Ruzuku kutoka kwa Washirika wa Maendeleo cha TZS 79.0 bilioni na makadirio ya matumizi ya TZS 1,829.9

bilioni, kinaonesha kushuka zaidi kwa kiwango cha utegemezi wa Bajeti na kufikia asilimia 4.3 kwa mwaka 2021/2022 kutoka asilimia 5.2 iliyoripotiwa mwaka uliopita. Hali hii inaonesha kuimarika kwa hali ya kujitegemea wenyewe kibajeti. Mchanganuo wa maeneo makuu ya Bajeti yanaonekana katika **Jaduweli Nam 4.**

Jadweli Nam 4: Makadirio ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2021/2022

	Makadirio ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2021/22		
			TZS Bilioni
	MAPATO SERIKALI KUU		
A	**Mapato ya Ndani**		**1,134.9**
	Mapato ya ZRB	525.1	
	Mapato ya TRA	413.1	
	Mapato yasiyokuwa ya Kodi	175.7	
	PAYE Transfer from SMT	21.0	
B	**Misaada na Mikopo Kutoka kwa washirika wa Maendeleo**		**383.0**
	Marejesho ya matumizi ya Mkopo Terminal III kutoka SMT	80.0	
	4.5% Msaada wa Kibajeti	20.0	
	Ruzuku	65.5	
	Mikopo nafuu ya miradi ya kisekta	204.0	
	Mfuko wa Pamoja wa Wafadhili	13.5	
C	**Mikopo ya Ndani na Nje**		**312.0**
	Mkopo wa Serikali kwa Miradi ya Maendeleo	220.0	
	Mikopo ya Hati Fungani	92.0	
	JUMLA YA MAPATO YA SERIKALI KUU (A+B+C)		**1,829.9**
D	**Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa**		
	Mapato ya Tozo na Ada	15.7	
	JUMLA YA MAPATO MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA(D)		**15.7**
	JUMLA KUU		**1,845.6**
	MATUMIZI SERIKALI KUU		
E	**Matumizi ya Kawaida**		**947.1**
	Mshahara Mawizara	364.9	
	Mshahara Ruzuku	76.8	
	Matumizi Mengineyo Mawizara	200.2	
	Matumizi Menginiyo Ruzuku	97.5	
	Mfuko Mkuu wa Serikali	207.7	
F	**Matumizi ya Maendeleo**		**882.8**
	Fedha kutoka Serikalini	606.5	
	Mikopo kwa Washirika wa Maendeleo	204.0	
	Ruzuku Kutoka kwa Washirika wa Maendeleo	72.3	
	JUMLA MATUMIZI YA SERIKALI KUU(E+F)		**1,829.9**
G	**Matumizi ya Mamlaka za Serikali ya Mitaa**		
	Matumizi ya Serikali za Mitaa kwa Makusanyo yao ya Ndani	15.7	
	JUMLA MATUMIZI YA MSM(G)		**15.7**
	JUMLA KUU		**1,845.6**

Chanzo: Ofisi ya Rais Fedha na Mipango

IX. MWELEKEO WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2021/22 -2023/24

126. Mheshimiwa Spika, Mwelekeo wa hali ya uchumi wa Zanzibar kwa mwaka 2021 unategemea kwenda sambamba na utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya 2050, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020-2025 na Mpango wa Maendeleo wa muda wa kati wa Zanzibar 2021-2025.

127. Mheshimiwa Spika, Pato la Taifa lilitarajiwa kukua kwa kasi ya wastani wa baina ya asilimia 5.0 – 7.1 kwa mwaka 2021 kutokana na matarajio ya kuongezeka kwa shughuli mbali mbali za maendeleo ikiwemo kuanza miradi mikubwa ya kipaumbele na maendeleo, kuwa na Sera nzuri na jumuishi za uwekezaji pamoja na kuweka mifumo imara ya ukusanyaji kodi. Hata hivyo, kutokana na kuendelea kuwepo kwa janga la ugonjwa wa COVID 19, uchumi wa Zanzibar unatarajiwa kukua kwa kasi ya chini ya asilimia 5.2. Hii ni kutokana na kuyumba kwa sekta za uchumi ikiwemo utalii, biashara na uwekezaji.

A. Shabaha na Malengo ya Uchumi kwa Mwaka 2021-2023

128. Mheshimiwa Spika, Shabaha na malengo ya uchumi kwa kipindi cha miaka mitatu inategemewa kuwa na misingi ifuatayo;

Shabaha za Msingi

a. Uwajibikaji katika kazi;
b. Kuendelea kuwajengea uwezo wafanyakazi;
c. Kuimarisha utawala bora;
d. Kutengeneza mifumo bora ya usimamizi wa makusanyo ya kodi;
e. Kuendelea kuweka sera bora na za kiushindani za uwekezaji;
f. Kuondoa ubadhirifu wa Mali za Umma, Wizi, Rushwa Uzembe, pamoja na;
g. Kuwepo kwa amani na utulivu.

Shabaha za Kiuchumi

a. Kasi ya ukuaji wa Pato la Taifa inategemewa kukua baina ya asilimia 5.0 - 7.1;
b. Kuendelea kudhibiti kasi ya mfumko wa bei kuwa katika wastani wa chini ya asilimia tano (5);
c. Mapato ya ndani kwa kipindi cha miaka mitatu yanakadiriwa kufikia wastani wa asilimia 39.2 ya Pato la Taifa kwa mwaka 2021/22-2023/24 kutoka asilimia 26.4 kwa mwaka 2020/21;
d. Kwa kipindi cha miaka mitatu nakisi ya bajeti kwa Pato la Taifa inakadiriwa kuwa chini ya asilimia 3 ifikapo mwaka 2023 hii ni kutokana na kigezo kilichowekwa na Jumuia ya nchi za Afrika Mashariki na SADC kuzitaka nchi wanachama nakisi zao kuwa chini ya asilimia 3.0;
e. Matumizi ya Serikali kwa Kipindi cha miaka mitatu inakadiriwa kufikia wastani wa asilimia 44.4 ya Pato la Taifa kwa mwaka 2021/22-2023/24 kutoka asilimia 39.4 kwa mwaka 2020/21 na
f. Utegemezi wa Bajeti unakadiriwa kubaki kwa wastani wa asilimia 2.4.

Shabaha Nyenginezo

a. Kuendelea kuwepo kwa amani na utulivu duniani;
b. Kuendelea kuwa na uhusiano mzuri na nchi Jirani;
c. Kupanda kwa thamani ya bidhaa za kusafirisha duniani ikiwemo karafuu na mwani;
d. Kuongezeka kwa uzalishaji na uwekezaji katika kanda ya Afrika Mashariki;
e. Kushuka kwa bei za Nishati katika soko la Dunia;
f. Kuendelea kupatikana kwa chanjo ya COVID19; na
g. Kuwepo kwa masharti nafuu ya kufunguliwa mipaka Duniani.

129. **Mheshimiwa Spika,** Mfumo kamili wa Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha miaka mitatu kwa mwaka 2021/2022-2023/2024 ni kama unavyonekana. **Katika jadweli Nam 5.**

Jadweli Nam 5: Mfumo wa Bajeti kwa kipindi cha Miaka Mitatu

MFUMO WA BAJETI KWA MWAKA 2021/2022-2023/2024						
					Tarakimu kwa TZS Bilioni	
Maelezo	**Makisio 2020/21**	**Matarajio 2020/21**	**Makisio 2021/22**	**Makisio 2022/23**	**Makisio 2023/24**	**% ya Bajeti**
MAPATO						
Mapato ya Ndani	1,050.0	769.7	1,134.9	1,291.4	1,445.8	73.3
Marejesho ya Mkopo	61.0		80.0			-
Mikopo na Ruzuku kutoka Nje (ODA)	423.2	154.0	283.0	277.1	291.8	36.4
4.5% Misaada ya kibajeti	100T		20.0			
Mkopo wa Ndani	45.0	101.2	92.0	40.0	60.0	224.9
Mkopo wa Serikali kwa Miradi ya Maendeleo			220.0	276.3	90.6	
Jumla ya Mapato	**1,579.2**	**1,024.9**	**1,829.9**	**1,884.8**	**1,888.2**	64.9
MATUMIZI						
Matumizi ya Kawaida	***969.3***	***733.6***	***947.1***	***1,046.9***	***1,181.0***	***75.7***
Mshahara Mafungu	316.8	276.0	364.9	421.4	450.9	***87.1***
OC Mafungu SMZ	182.6	85.6	200.2	218.7	277.3	46.9
Mfuko Mkuu wa Serikali	237.9	167.9	207.7	224.3	238.2	70.6
Mshahara Ruzuku	123.8	132.3	76.8	77.2	82.6	106.9
OC Ruzuku	108.2	71.8	97.5	105.3	132.0	66.4
Matumizi ya Maendeleo	***609.9***	***291.3***	***882.8***	***837.9***	***707.2***	47.8
Fedha za SMZ	197.3	137.3	606.5	561.5	416.1	69.6
Mikopo na Ruzuku kutoka Nje (ODA)	412.6	154.0	276.3	276.4	291.1	37.3
Jumla ya Matumizi	**1,579.2**	**1,024.9**	**1,829.9**	**1,884.8**	**1,888.2**	**64.9**

Chanzo: Ofisi ya Rais Fedha na Mipango

X. VIPAUMBELE VYA KITAIFA KWA MWAKA 2021/2022

130. Mheshimiwa Spika, Vipaumbele vya Kitaifa na mwelekeo wa Serikali unazingatia katika maeneo yafuatayo;

i. Kuimarisha maendeleo ya Rasilimali Watu na Utawala Bora;

ii. Kusimamia matumizi sahihi ya ardhi na kupima maeneo yote kwa ajili Makaazi, Viwanda, Kilimo na Uwekezaji;

iii. Kuimarisha miundombinu ya upatikanaji wa Huduma za Jamii ikiwemo Afya, Elimu na huduma za Maji;

iv. Kuendeleza utafutaji wa Nishati mbadala ya Umeme na Kutambua matumizi na mahitaji halisi ya Madini Zanzibar;

v. Kuendeleza maeneo ya Historia kwa kufanya utafiti wa kujua historia za Majengo na kuendelea na mpango wa kuingiza masomo ya uhifadhi katika mitaala ya kufundishia kuanzia

elimu ya msingi hadi vyuo vikuu;

vi. Kujenga uchumi wa kisasa kwa kubadilisha mfumo wa matumizi ya rasilimali ya bahari, shughuli za Utalii, na Uwekezaji;

vii. Kusimamia kwa karibu masuala ya udhalilishaji wa kijinsia;

viii. Kuimarisha utawala bora kwa kupambana na vitendo vya rushwa na uhujumu wa Uchumi;

ix. Kuimarisha, sekta ya usafirishaji na mawasiliano ya anga, baharini na nchi kavu ili kuwa kichocheo cha kukuza uchumi katika nchi yetu; na

x. Kukuza uchumi na kuimarisha maslahi ya Wananchi.

XI. SHUKURANI

131. Mheshimiwa Spika, Kwa kumalizia hotuba yangu naomba kuchukua fursa nyengine kumpongeza tena Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi kwa namna alivyoweza kutekeleza shughuli za Serikali kwa utaratibu anaoutumia kwa kufuatilia kwa vitendo shughuli hizo. Uwajibikaji, uadilifu, dira na busara zake zinawezesha mafanikio makubwa yanayoendelea kupatikana katika utekelezaji wa majukumu ya Serikali kwa ujumla. Hali hii imetupa changamoto sisi viongozi kubuni namna bora ya kuwatumikia wananchi. Namuomba Mwenyezi Mungu ampe nguvu na siha kuweza kufikia adhma na dhamira yake kwa ufanisi na mafanikio.

132. Mheshimiwa Spika, Shukurani zangu za dhati, kwako wewe binafsi Spika wa Baraza la Wawakilishi Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid kwa kuliongoza vyema na kwa uweledi Baraza hili tukufu. Vilevile na wapongeza Naibu Spika Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma na Wenyeviti wa Baraza Mheshimiwa Shabaan Ali Othman na Mhe Mwanaasha Khamis Juma kwa uongozi wao mzuri. Kadhalika, nachukua Fursa hii kumpongeza kwa dhati Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir Mrembo kwa kuteuliwa kwake kwenye Kamati hii, uweledi na umahiri wake utasaidia

sana katika kuongoza Kamati hii muhimu. Aidha nachukua nafasi hii kumpongeza Makamo Mwenyekiti pamoja na wajumbe wote wa kamati kwa umakini wao katika kuongoza shughuli za kamati, msaada na miongozo yao kwangu binafsi na kwa watendaji wa Ofisi yangu imesaidia sana Serikali kuimarisha ufanisi wa kiutendaji wa majukumu ya Serikali, Aidha, ninawapongeza Wenyeviti, Makamu wenyeviti na wajumbe wa Kamati zote za Kudumu za Baraza hili tukufu kwa mashirikiano, maoni na miongozo yao katika kipindi chote cha maandalizi ya bajeti hii ninayoiwasilisha mbele yenu. Ushauri, mapendekezo na maelekezo yao waliyokuwa wakiyatoa kupitia kamati na vikao mbali mbali katika kuboresha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara mbalimbali na Serikali yamesaidia kwa kiwango kikubwa kuikamilisha bajeti hii kwa ufanisi.

133. **Mheshimiwa Spika,** Shukrani zangu mahsusi nazielekeza kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, Dkt. Juma Malik Akil, Naibu Katibu Mkuu Fedha na Mipango Bwana Khamis Suleiman Mwalim na Naibu Katibu Mkuu TEHAMA Bwana Rashid Said Rashid, Naibu Mhasibu Mkuu wa Serikali, Kamishna wa Bajeti, Mkurugenzi wa Sera za Kodi na Fedha, pamoja na Makamishna, Wakurugenzi, na watendaji wote wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kwa mashirikiano na mshikamano wao mzuri hadi kukamilisha zoezi hili la mchakato wa Bajeti ya Serikali. Bajeti hii isingekamilika bila ya mchango wa watendaji wakuu na wafanyakazi wote wa Wizara na Idara za Serikali; nao wote kwa pamoja nawapa shukrani zangu za dhati.

134. **Mheshimiwa Spika,** Kwa heshima na Taadhima naomba nikishukuru chama changu Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa kuniamini, kunipendekeza na kuniteuwa kuwa Mgombea wa Jimbo la Magomeni na kwa umuhimu wa pekee sasa natoa shukurani zangu za moyoni kwa Wananchi wa Jimbo langu la Magomeni kwa Imani kubwa na upendo wanaoendelea kunipatia.

135. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa uongozi ni dhamana na dhamana ni deni sisi kama viongozi tunaahidi kubeba dhamana hii kwa kufuata maelekezo yote tutakayopewa na viongozi wetu kwa bidii, utii na uadilifu ili kulipa deni hili kwa nchi yetu. Ni muhimu sana watendaji na wananchi wote kwa pamoja kuzidisha moyo na ari ya kujituma kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu.

136. **Mheshimiwa Spika,** Naomba kuwatambua na kuwashukuru Nchi rafiki na washirika wetu wa kimaendeleo wanaotarajia kuchangia Bajeti yetu ya Serikali kwa mwaka 2021/2022, zikiwemo nchi za Canada, Cuba, Denmark, Finland, India, Ireland, Japan, Jamhuri ya watu wa China, Hispania, Korea ya Kusini, Kuwait, Malaysia, Marekani, Misri, Norway, Oman, Qatar, Saudi Arabia, Sweden, Uingereza, Ujerumani, Umoja wa Falme za Kiarabu na Uturuki.

137. **Mheshimiwa Spika,** Nachukua fursa hii kuwashukuru na kuthamini msaada na mashirikiano ya Mashirika ya Ndani na Nje yanayotarajiya kutusaidia Bajeti yetu ya Serikali naomba niyataje kama ifuatavyo:- Africa Development Bank (AfDB), Global Fund (GF), BADEA, IFAD, JICA, KOICA, NORWAY,UNDP, UNICEF, World Bank (WB), Exim Bank, Global Partner Ship for Education(GPE) United State Agency for International Development (USAID), European Union (EU), United Nation Population fund (UNFPA), Saudi Fund (SF), United Nation For Women (UN Women), World Diebatic foundation (WDF), Khalifa Fund (KF) , Global Fund (GF), Korea, MILELE NORAD, UNESCO, Partnership for Child Development International Atomic Energy Agency(IAEA) United Arab Emirate (UAE), Nutrition International (NI),CROWN, Schistomasiss Contol Initiative(SCI), United Nation Environment Programme (UNEP),Taasisi Inayosimamia Watoto Yatima Qatar (QCO), na Table for Two (TFT).

XII. HITIMISHO

138. Mheshimiwa Spika, Mwisho kabisa, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe Makadirio ya Mapato ya Serikali ya kukusanya jumla ya Shilingi Trilioni Moja, Bilioni Mia Nane na Ishirini na Tisa na Milioni Mia Tisa (TZS 1,829.9 bilioni) kwa mwaka wa fedha, 2021/2022. Kati ya mapato hayo, mapato ya ndani ni TZS 1,134.9 bilioni, Ruzuku na Mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo TZS 283.0 bilioni, mikopo ya Ndani na Nje kwa ajili ya kugharamia Miradi ya Maendeleo TZS 312.0 bilioni, TZS 80 bilioni ni Marejesho ya matumizi ya Mkopo Terminal III kutoka SMT na TZS 20 bilioni zinatokana na Misaada ya Kibajeti.

139. Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa matumizi, nina heshima ya kuliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya shilingi Trilioni Moja, Bilioni Mia Nane na Ishirini na Tisa na Milioni Mia Tisa (TZS 1,829.9 bilioni) kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Kati ya matumizi hayo TZS 947.1 bilioni ni kwa ajili ya kazi za kawaida na TZS 882.8 bilioni kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo.

140. Mheshimiwa Spika, Naomba kutoa hoja.

JAMAL KASSIM ALI (MBM),
WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS FEDHA NA MIPANGO, ZANZIBAR.
JUNI 2021.

PROGRAMU/MIRADI YA MAENDELEO CHINI YA MFUKO WA MIUNDOMBINU (INFRASTRUCTURE FUND)		
FUNGU	**JINA PROGRAMU/MIRADI**	**MAKISIO YA 2021/22 ("000")**
P01	**WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI**	
	Programu ya Ujenzi wa Barabara	
	i) Barabara ya Chake Chake-Wete (km 22.1)	8,000,000
	ii) Barabara ya Jumbi Sokoni - Tunguu (km 4)	10,200,000
	iii) Barabara ya Fumba - Kisauni (km12)	1,000,000
	iv) Barabara ya Finya - Kicha (km 8.8)	8,000,000
	v) Ujenzi wa Misingi ya Kuondoshea Maji katika Barabara (km 30.5)	5,000,000
	vi) Ujenzi wa Bandari Jumuishi - Mangapwani	3,000,000
	vii) Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba	2,000,000
	JUMLA YA FUNGU	**37,200,000**
N03	**WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI**	
	i) Mradi wa Uendelezaji wa Visima	7,273,517
	ii) Mradi wa Usambazaji Umeme Vijijini	2,000,000
	JUMLA YA FUNGU	**9,273,517**
	JUMLA KUU	**46,473,517**